



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb:HWR/K.2/VOL.IV/12/106

23/05/2022

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 51,
Ruungwa

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruungwa anayo furaha ya kutangaza nafasi 22 za ajira ya kudumu kwa Watanzania wenye sifa stahiki ikiwemo **Mtendaji wa kijiji Daraja la III** na **Katibu Mahsusi Daraja la III**. Nafasi za ajira hizi zinatokana na kibali cha ajira kutoka kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora** kwa barua yenye **Kumb. Namba FA.97/228/01/9** ya tarehe **13 Mei, 2022**

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III-(NAFASI 18)

A. Sifa za mwombaji:

- Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne (IV) au Sita (VI) pia awe amehitimu mafunzo ya cheti/ Astashahada "NTA Level 5" katika moja ya fani zifuatazo:-
- **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa** kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

B. KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDA WA KIJIKI III

- Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya
- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani, Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu

- kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaaluma katika ngazi ya kijiji
- kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Serikali ya kijiji
- Mwenyekiti wa kikao cha Wataalam waliopo katika kijiji
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata
- Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri

C. Ngazi ya Mshahara ni TGS B.

2. KATIBU MAHSUSI III – (NAFASI 4)

A. Sifa za mwombaji:

- Awe amehitimu kidato cha IV/VI
- Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu
- Awe amefaulu somo la hati mkato ya kiswahili na kiingereza maneno 80 kwa dakika moja
- Awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, Email na Publisher.

B. KAZI NA MAJUKUMU YA KATIBU MAHSUSI III

- Kuchapa barua, taarifa za kawaida
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, tarehe za vikao, Safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi nyingine zilizopangwa kutekeleza katika Ofisi anaefanyia kazi na kumwalifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika
- Kusaidia kufanya na kumpatia mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote katika shughuli za kazi hapo Ofisini
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa anapewa na wasaidizi hao
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika na
- Kazi nyingine atakazopangiwa na mwajiri.

C. Ngazi ya Mshahara ni TGS B


3. MASHARTI YA JUMLA

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa, maelezo binafsi (CV) na nyaraka zote muhimu pamoja na picha mbili (2) (Passport size) zilizopigwa hivi karibuni.
- Testimonials "provisional results" "statement results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (**FORM FOUR AND FORM SIX RESULTS SLEEPS**) **HAVITAKUBALIWA**
- Nafasi ya kazi iliyoombwa iandikwe juu ya bahasha, kutozingatia hii kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili
- Kwa wale watakaopita kwenye mchujo wa awali (short listened candidates). Ndio watakaoitwa kwenye usaili (interview) na kufika na vyeti halisi.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa Mkono na kutumwa kwa njia ya posta kwa anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA,
S.L.P 51,
RUANGWA

NB; Uwasilishaji wa barua za maombi kwa mkono katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya hazitapokelewa.

Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe 08 Juni, 2022 saa 9:30 Alasiri.



George R. Mbesigwe
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
RUANGWA

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR,
RUANGWA DISTRICT COUNCIL
P. O. Box 51,
RUANGWA